

OFISI YA RAIS- TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE,
S.L.P 479,
NJOMBE.

KUMB. NO. MKSS / JOIN. INS/2021/VOL 01

Mawasiliano :0768661887(MKUU WA SHULE)

MZAZI/MLEZI WA -----

SHULE YA MSINGI -----

NJOMBE.

YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE MWAKA 2021.

1. Napenda kukujulisha kuwa mtoto wako amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii – 2021
2. Natumia nafasi hii kukupongeza kwa kupata nafasi adimu.
3. Mzazi/mlezi hakikisha unakuja na mwanao tarehe **11/01/2021 siku ya jumatatu saa mbili kamiili asubuhi kwa lengo la kumuandikisha shule kumbuka hili ni agizo kutoka serikalini.**
4. Shule hii ni ya hosteli ipo katika kijiji cha Kipengere, kata ya Kipengere, Tarafa ya Imalinyi wilaya ya wanging'ombe. Wanafunzi wote wanakaa hosteli.
5. Kabla ya kupokelewa shuleni mwanafunzi anatakiwa kupimwa na daktari ili kuthibisha afya yake ambapo atajaza fomu maalumu iliyoambatanishwa na barua hii.
6. Pamoja na barua hii naambatanisha mambo yafuatayo:
 - Fomu ya kujiunga/kujiandikisha shuleni.
 - a) Maagizo mbalimbali.
 - b) Fomu ya daktari.

MUHIMU KUZINGATIA: Fomu Na (b) na (c) ijazwe na kurudishwa shuleni siku ya kuripoti.

Mzazi /mlezi hakikisha unakuja na mwanao na sio kuagiza

HONGERA KWA KUPATA NAFASI HII ADIMU NA KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE,

“ELIMU KWA KUONDOA UMASKINI”

MHANGA B.B

MKUU WA SHULE

MAAGIZO MBALIMBALI VIFAA NA FEDHA.

1. SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

- i. Suruali pair mbili moja darkblue na nyingine damu ya mzee
- ii. Mashati mawili (02) meupe mikono mifupi.
- iii. Viatu vya ngozi nyeusi vyenye soli fupi na soksi rangi nyeusi
- iv. Sweta ya (blue) lenye muundo wa **V**-shingoni
- v. Tai mbili. moja darkblue na nyingine damu ya mzee
- vi. Nguo za ndani za kutosha
- vii. Suruali nyeusi kwa ajili ya kazi za nje.
- viii. Raba kwa ajili ya michezo
- ix. Track suti nyeusi yenye michirizi rangi nyeupe kwa ajili ya michezo
- x. **Jaketi jeusi lisilokuwa over size**

B. WASICHANA.

- i. Blauzi mbili (02) nyeupe za mikono mifupi.
- ii. Suruali peya (pair) mbili moja ya kitambaa cha damu ya mzee na nyingine dark blue:
- iii. Sketi pair mbili zinazoishia kwenye magoti kitambaa cha damu ya mzee na nyingine zambarau
- iv. Soksi nyeupe zisizopungua pea tatu (03)
- v. Sweta la (**blue**) lenye muundo wa **V**-shingoni
- vi. Gauni la kijani kwa ajili ya kazi za nje linalofika karibia na kisigino.
- vii. Viatu vyeusi pair mbili vyenye soli fupi vya kamba
- viii. Tai mbili moja darkblue na nyingine damu ya mzee
- ix. Raba za michezo
- x. Track suti nyeusi yenye michirizi rangi nyeupe kwa ajili ya michezo
- xi. Nguo za ndani za kutosha
- xii. **Jaketi jeusi lisilokuwa oversize.**

C: VIFAA VYA BWENINI KWA WOTE:

Ndoo moja, godoro moja size ya mbili na nusu kwa sita, shuka mbili rangi moja blue bahari na pinki, blanketi zito, taulo, nguo za ndani za kutosha, sabuni, dawa ya meno, mafuta ya kupakaa, kitana, kioo, kiwi, ndala za kuogea, mwavuli, tranker au sanduku imara la chuma.

D. VIFAA VYA DARASANI

Daftari counter book quire 3 ziwe 10, na daftari ndogo za kati kwa ajili ya mazoezi ziwe 10, peni za blue au nyeusi, mkebe, rula, Kalamu ya mkaa.

Rimu moja (**A4**) au bunda la karatasi moja

E: MCHANGO WA CHAKULA: Aidha nachukua fursa hii kukujulisha mzazi/mlezi kuwa shule ni ya kutwa na si bweni hivyo kuwepo na hostel au vyumba vya kulala wanafunzi ni mpango wa wazazi na uongozi wa shule, hivyo kila mzazi atawajibika kumgharamia mwanaye kuishi hostel kwa kuchangia chakula, aidha ieleweke kwamba mchango huu wa chakula si ada ya masomo kama ilivyozoeleka bali ni kumuwezesha mwanao kuishi shuleni badala ya kuishi nyumbani au kupanga; **KWA MAANA HIYO MCHANGO WA CHAKULA UTAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

1. **MAHINDI DEBE 12** kwa mwaka na tunashauri kuleta debe sita kwa muhula wa kwanza na debe sita muhula wa pili
2. **MAHARAGE DEBE 02** kwa mwaka na tunashauri kuleta debe 1 kwa muhula wa kwanza na debe 1 muhula wa pili
3. **MCHELE DEBE 1 AU KILO ISHIRINI:** angalizo. mchele utapokelewa ule wa grade ya kwanza na pili tu, ili kulinda afya za watoto, pia tunashauri kuleta kilo 10 kwa muhula wa kwanza na kilo 10 muhula wa pili

4. MCHANGO WA FEDHA YA CHAKULA: Kila mzazi utatakiwa kuleta kiasi cha **TSH: 100,000/=** kwa wale wanafunzi wa ndani ya kata tu na wale wanaotoka nje ya kata watatakiwa kulipa **Tsh 170,000/=** kwa mwaka, fedha hii ni kwa ajili ya kununua sukari, chumvi, mafuta ya kupikia, kukoboa na kusaga nafaka, matengenezo ya mashine, kulipa wapishi, kununua kuni, kununua nyama, kununua vifaa vya jikoni kama vile masufulia nk, kumlipa matron pamoja na kutengeneza vitanda. **HIVYO KILA MZAZI/MLEZI NI MUHIMU KULIPA MICHANGO HIYO KWA AWAMU MBILI NUSU MUHULA WA KWANZA NA KIASI KINACHOBAKI MUHULA WA PILI**

Fedha ya chakula ilipwe kwa kukupitia akaunti ya shule ambayo ni **60601000017 NMB** Mount kipengere secondary school revenue collection.

NB FEDHA YA MCHANGO WA HOSTERI ILIPWE KUPITIA AKAUNTI YA SHULE NA SIO KULETA KESHI SHULENI

FOMU NA F2. KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA
(IJAZWE NA MZAZI AKISHIRIKIANA NA MWANAFUNZI)

SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULE.

- A. Jina la kwanza -----
Jina la baba -----
Jina la ukoo -----
Dini -----
Msichana/mvulana -----
Tarehe ya kuzaliwa -----
Mahali/wilaya ulipozaliwa -----
Shule ya msingi uliyofanya mtihani wa darasa la saba -----
Kama ulihamishiwa kutoka shule nyingine ya sekondari jina na anwani ya shule hiyo -----

Nathibitisha kuwa taarifa niliyojaza hapo juu ni sahihi

Sahihi ya mzazi / mlezi


Tarehe

AHADI YA MWANAFUNZI

- 1) Mimi (jina la mwanafunzi) ----- nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote na sheria na taratibu za shule na nimekubali kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mount Kipengere kuanzia tarehe ----- hadi nitakapomaliza kidato cha nne.
- 2) Kwa hiyo naahidi kwamba
 - a) Nitazitii sheria za shule na kutimiza mambo yote yaliyoelekezwa.
 - b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa chama Tawala ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
 - c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengona samani (**furniture**) vitabu n.k

Sahihi ya mwanafunzi

Tarehe



Sketi mbili, moja rangi ya **damu ya mzee** na nyingine **zambarau** zinazoishia kwenye magoti.

Suruali mbili, moja rangi ya **damu ya mzee** nanyingine **Dark blue**.

Mchoro: Muundo wa vazi kwa wasichana chini ya tumbo.

FOMU NA F3. MEDICAL EXAMINATIONS

(To be completed by medical officer)

- 1. Pupil's name.....
- 2. Age.....
- 3. Blood count (white and red).....
- 4. Stool examination.....
- 5. Syphilis or/and other venereal diseases test.....
- 6. T.B test.....
- 7. Eye test.....
- 8. Ears.....
- 9. Abdomen.....
- 10. Spleen.....
- 11. Urine for plamo test.....

ADDITIONAL INFORMATION

If any e.g. physical defects, impairment, infections, pregnancy, chronic or family diseases
etc.....
.....

I CERTIFY THAT HTE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION

Station..... Signature.....

Date..... Designation.....

.....